**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SINGIDA**

MKOA WA SINGIDA
Anuani:"AFYA

Simu Na: 026-2502397
Fax Na: 026-2502360
E.mail: singidarrh@afya.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

HOSPITALI YA RUFAA MKOA
S.L.P. 104,

**SINGIDA.**

**Kumb. MB.22/427 /01/64** **16/06/2023**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida kupitia Wizara ya Afya anawatangazia nafasi 04 za kujitolea kwa waombaji wenye sifa katika kada zifuatazo:-

| NA | KADA | NAFASI | SIFA |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisa Habari Daraja la II | 1 | Mwombaji awe na sifa zifuatazo: -<br>- Awe na shahada ya kwanza au stashahada ya juu ya Uandishi wa Habari au sifa nyingine inayofanana na hiyo kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Serikali<br>- Awe na Elimu ya Kidato cha nne / sita<br>- Awe Raia wa Tanzania na ambaye hajawahi kushtakiwa kwa makosa ya jinai<br>- Awe na Umri usiozidi miaka 35<br>- Awe amesajiliwa na kupatiwa kitambulisho cha Taifa (NIDA)<br>- Mwenye uzoefu wa kazi na uwezo wa kutumia program ya graphics and Design atapewa kipaumbele |
| 2 | Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II | 1 | Mwombaji awe na sifa zifuatazo: -<br>- Awe na cheti cha Mafunzo ya Dawa za Usingizi na Ganzi<br>- Awe amehitimu stashahada ya Uuguzi<br>- Awe na Leseni ya Uuguzi iliyohuishwa na amesajiliwa katika Baraza la Uuguzi na Ukunga<br>- Awe na Elimu ya Kidato cha nne / sitta<br>- Awe Raia wa Tanzania na ambaye hajawahi kushtakiwa kwa makosa ya jinai |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | - Awe na Umri usiozidi miaka 35<br>- Lazima awe amesajiliwa na kuwa na kitambulisho cha Taifa<br>- Mwenye uzoefu wa kazi na uwezo wa kutumia kompyuta atapewa kipaumbele |
| 3 | Msaidizi wa Afya | 1 | Mwombaji awe na sifa zifuatazo: -<br>- Awe amehitimu kidato cha nne kupata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya / Afya ya Jamii kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali<br>- Awe na Elimu ya Kidato cha nne<br>- Awe Raia wa Tanzania na ambaye hajawahi kushtakiwa kwa makosa ya jinai<br>- Awe na Umri usiozidi miaka 35<br>- Awe amesajiliwa na kupatiwa kitambulisho cha Taifa (NIDA)<br>- Mwenye uzoefu wa kuendesha mashine ya kichomea taka atapewa kipaumbele |
| | **Jumla ya Nafasi** | **3** | |

2. Waombaji waambatishe vivuli vya cheti cha kuzaliwa,vyeti vya Elimu na Taaluma ,CV, na kivuli cha kitambulisho cha NIDA, leseni na vyeti vya usajili vya Baraza la Uuguzi na Ukunga kwa wale watakaoomba nafasi ya Muuguzi Msaidizi.

3. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:

**Mganga Mfawidhi**

**Hospitali ya rufaa ya Mkoa**

**S.L.P 104**

**SINGIDA**

**Au**

Wasilisha maombi yako Masijala iliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

4. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 26/06/2023 Saa 9: 30 alasiri.

5.Tangazo hili limetolewa na:-

Dkt. Muhaji K. Mohamed

Mganga Mfawidhi

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa

SINGIDA

MEDICAL OFFICER INCHARGE
SINGIDA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL,
P. O. Box 104
SINGIDA